
GOVERNMENT OF WESTERN AUSTRALIA

**Roll up for WA**
COVID-19 Vaccination

# Pata ukweli juu ya chanjo




Ni kawaida kuwa na maswali kuhusu mambo mapya. Gundua nini ni kweli na nini sio kweli kuhusu chanjo za COVID-19. Pamoja, tunahitaji kujenga ujasiri wa chanjo kwa sababu kila mtu aliyechanjwa anatusaidia kuweza kupita janga hili.

## UKWELI

**Chanjo ni salama**
Watu wengi duniani walifanya kazi pamoja kutengeneza chanjo za COVID-19, kushirikiana fedha na wanasayansi ili kuifanya katika miezi tu, bila kukosa hatua zozote. Chanjo zinaruhusiwa tu nchini Australia baada ya kupimwa na kubainika kuwa salama na ufanisi. Chanjo zote zinaendelea kupimwa kwa ubora na kufuatiliwa kwa usalama.

**Chanjo za COVID-19 hazina virusi hai na haziwezi kukupa ugonjwa wa COVID-19**
Chanjo hizo zinajifanya kuwa virusi halisi na hufundisha mwili wako jinsi ya kujilinda wenyewe. Hii itasaidia kukuzuia kupata kuumwa sana na kulazwa hospitali au hata kufariki.

**Microchip isingeweza kupita sindano ya chanjo**
Habari potofu hii imetokana na video ya uongo inayozunguka mtandao wa jamii.

## HABARI POTOFU

- Chanjo za COVID-19 ziliidhinishwa haraka sana hivyo haziwezi kuwa salama.
- Chanjo za COVID-19 zingeweza kukupa ugonjwa wa COVID-19.
- Chanjo za COVID-19 zina microchip ndani ili kunifuata.

# Pata ukweli juu ya chanjo

## UKWELI

### Chanjo ni bure kwa kila mtu katika WA
Hii inajumuisha wakazi wa muda, wakimbizi, wahamiaji na watu wasio na viza halali.

### Tunajua kila kiungo ambacho kimo ndani ya chanjo hizi
Chanjo hizi kwa kiasi kikubwa ni maji, pamoja na chumvi, sukari na mafuta. Hakuna bidhaa za oksidi ya graphene, gluten, yai, ngano, sumu ya nyuki, mpira au za wanyama katika chanjo zile. Baraza la Fatwa la Australia limeidhinisha chanjo hizo kama Halal.

### Unaweza kupata chanjo ya COVID-19 hata ikiwa huna Medicare
Utahitaji kuthibitisha kitambulisho chako katika miadi yako, kwa hiyo tafadhali leta waraka iliyo na jina lako kama leseni ya dereva, barua au barua ya gharama.

### Kupokea chanjo ya COVID-19 hakusababishi wewe kuwa sumaku - popote kwa mwili wako
Chanjo za COVID-19 hazina viungo vyovyote vya sumaku ndani ambavyo vingeweza kufanya hivi. Ungalihitaji metali nyingi ili kuvuta sumaku. Kwa mfano, watu wanatumia vitamini nyingi ambavyo mara kwa mara vina chuma ndani. Hii haisababishi hawa kuwa sumaku kwa sababu vinazama sana na kuenea sana katika mwili wako.

### Chanjo za COVID-19 haziathiri uzazi
Chanjo haziathiri uwezo wako wa kupata mtoto sasa, au kwa baadaye. Pia inashauriwa sana kuwa wanawake wajawazito wapate chanjo ya COVID-19 ili kujilinda na kulinda watoto wao.

## HABARI POTOFU

- ✗ Inagharimu fedha ili kupata chanjo ya COVID-19.
- ✗ Hatujui ni nini kilicho katika chanjo hizi.
- ✗ Unahitaji kuwa na kadi ya Medicare inayofanya kazi ili kupata chanjo ya COVID-19.
- ✗ Chanjo za COVID-19 zinaweza kusababisha sumaku kushikilia mkono wako.
- ✗ Chanjo za COVID-19 zinaathiri uzazi.

Jiandikishe na panga miadi kwa ajili ya chanjo yako ya COVID-19

rollupforwa.com.au

13COVID
(13 26843)
Bonyeza * kwa mkalimani